

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

## TANGAZO



### UTOAJI WA LESENI ZA VILEO KIPINDI CHA KUANZIA

**TAREHE 01/10/2018 hadi 31/03/2019**

(Chini ya Sheria ya Leseni za Vileo Na. 28 ya 1968 na marekebisho yake)

Wafanyabiashara wote mnaoendesa biashara ya Vileo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni mnatangaziwa kuwa, leseni za Vileo zilizotolewa kuanzia **tarehe 01/04/2018** muda wake unaishia **tarehe 30/09/2018** hivyo mnatakiwa kuleta maombi kwa kipindi kinachoanza **tarehe 01/10/2018** hadi **tarehe 31/03/2019**.

Fomu za maombi ya Leseni za Vileo, zinapatikana katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, Makao Makuu ya Manispaa iliyopo nyuma **ya Uwanja wa Mpira/Mkabala na Shule ya Msingi Mji Mwema**.

Fomu za maombi mapya na ya zamani, zijazwe kikamilifu na kurejeshwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Ofisi ya Biashara kabla ya tarehe **15/09/2018**: Fomu ya maombi yanayorudiwa (Renewal) iambatishwe na Tax Clearance na kivuli (Photocopy) cha leseni ya kipindi kinachoishia tarehe **30/09/2018**. Aidha, maombi mapya yaambatishwe vivuli (copy) vya TIN, nyaraka ya kiwanja au mkataba wa pango na kitambulisho cha Uraia au mpiga kura au passport.

- MWISHO:**
- (i) **Mamlaka ya Utoaji wa Leseni za Vileo ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, haitahusika kwa lawama yoyote itakayotolewa na mwombaji aidha kwa kuchelewesha maombi yake au kutokuzingatia tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa maombi na hivyo kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria.**
  - (ii) **Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayekutwa akiendesha biashara ya vileo bila ya leseni halali ya kipindi/vipindi husika.**
  - (iii) **Wafanyabiashara mnatahadharishwa kutokuwatumia mawakala au watu wasiohusika katika kushughulikia maombi ya leseni zenu.**

Ng'wilabuzu N. Ludigija  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
KIGAMBONI